# Mataifa yote watakusujudia




Ee Mungu, umpe mfalme hukumu yako;
na mwana wa mfalme haki yako;
ahukumu taifa lako kwa haki,
na wanyonge kwa usawa. (K)
Katika siku zake haki iendelee,
na amani izidi mpaka mwezi ukome.
Atawale toka bahari hata bahari,
na toka ule mto hata miisho ya dunia. (K)
Wafalme wa Tarshishi na visiwa watatoa kodi,
wafalme wa Sheba na Seba wataleta zawadi.
Wafalme wote wa dunia watamwangukia,
mataifa yote watamtumikia. (K)
Maana atamkomboa maskini mwenye kumlilia,
na mnyonge asiye na msaidizi.
Atamhurumia dhaifu na mhitaji,
na anayaokoa maisha ya wahitaji. (K)